

# Taliri kutatua changamoto ya mbegu bora za malisho

"Tafiti tunazozi-fanya zinalenga kulmarisha mnyororo wa thamani wa mifugo ili mchango wa sekta ya mifugo uweze kuonekana katika uchumi wa kati."

Kaimu  
Mkurugenzi  
Mkuu Taliri,  
Dk Jonas  
Kizima

Mwandishi Wetu, Mwananchi  
mwananchipapers@mwananchi.co.tz

**Mpwapwa.** Kaimu Mkurugenzi Mkuu, Taasisi ya Utafiti wa Mifugo Tanzania (Taliri), Dk Jonas Kizima amesema wamejikita kutatua changamoto za mbegu bora za mifugo na malisho.

Dk Kizima alisema hayo alipotembelea kukagua shughuli zinazofanywa na Kituo cha Taliri Mpwapwa, kilichopo wilayani hapa Mkao wa Dodoma juzi.

Alisema lengo la utafiti wanaufanya ni kuhakikisha wanapata mbegu bora za mifugo pamoja na kuzalisha mbegu bora za malisho ya mifugo zitakazosaidia kutatua changamoto za upatikanaji wa mbegu bora za mifugo zinazohimili mazingira yaliyopo.

Dk Kizima alisema kwa sasa, taasisi hiyo inaendelea kufanya tathmini ya ubora, ustahimilivu na makazi ya malisho ya mifugo yatakayofaa kwa chakula cha kutosha.

Mkurugenzi wa Idara ya Utafiti, Mafunzo na Huduma za Ugani, Dk Angello Mwilawa alisema Wizara ya Mifugo na Uvuvi imezihamasisha halmashauri zote nchini kuanzisha mashamba darasa ya malisho ili wafugaji wajifunze namna ya kupata mbegu bora za malisho kwa ajili ya mifugo.

"Tunawahimiza wafugaji kuona umuhimu wa kulima malisho ili yawsaidie kupata lishe ya uhakika kwa mifugo yao, pia kwa kulima malisho kutawapunguzia migogoro ya mara kwa mara katika yao na wakulima," alisema Dk Mwilawa.

Pia alisema wanawahamasisha wafugaji wa nyanda kame wastawishe malisho ya mifugo wakati wa masika na kuyatunza.

MWANANCHI  
20/2/2021

# Taliri yajikita katika mbegu bora za mifugo na malisho

HABARI LEO 20/2/2021  
Na Mwandishi Maalum, Mpwapwa

**K**AIMU Mkurugenzi Mkunu, Taasisi ya Utafiti wa Mifugo Tanzania (Taliri), Dk Jonas Kizima, amesema utafiti wanaoufanya umejikita kutatua changamoto za mbegu bora za mifugo na mbegu bora za malisho kwa wafugaji ili sekta ya mifugo ichangie vyema katika pato la taifa.

Aliysema hayo juzi alipokagua shughuli zinazofanywa na Kituo cha Taliri kilichopo wilayani Mpwapwa, Dodoma.

Alisema utafiti wanaoufanya unalenga kuhakikisha wanapata mbegu bora za mifugo na kuzalisha mbego bora za malisho ya mifugo zitakazosaidia kutatua changamoto za upatikanaji wa mbegu bora za mifugo zinazohimili mazingira yaliyopo na malisho inayoikabili nchi kwa sasa.

Aliongeza taasisi hiyo inaendelea kufanya tathmini ya ubora, ustahimilivu na makuzi ya malisho ya mifugo yatakayofaa kwa chakula cha kutosha kwa ajili ya mifugo.

Kwa mujibu wa Dk Kizima, matokeo yoyote ya utafiti lazima yabadilishwe kuwa biashara kwa sababu wafugaji wakifanya ufugaji unaocendana na mazingira yao, wataongeza tija katika ufugaji wao na kukuza uchumi.

"Tafiti tunazozifanya zinalenga kuimarisha mnynororo wa thamari wa mifugo ili mchango wa sekta ya mifugo uonekane katika uchumi wa kati," alisema.

Kizima alisema Taliri imesambaza vituo vyake katika kanda saba nchini ili kuwa karibu na wafugaji na kuwasaidia kutatua changamoto hali itakayowaweze-sha kufuga kwa tija.

Vituo hivyo viro katika kanda za Mashariki, Kaskazini, Kati, Kusini, Magharibi, Ziwa na Kanda ya Nyanda za Juu Kusini. Mkurugenzi, Idara ya Utafiti, Mafunzo na Huduma za Ugani, Dk Angello Mwilawa, alisema Wizara ya Mifugo na Uvuvi imezihamasisha halmashauri nchini kuanzisha mashamba darasa ya malisho ili wafugaji wajifunze na kupata mbegu bora za malisho kwa ajili ya mifugo.